


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



Anuani ya simu "ELIMU"
Simu: 026 296 35 33
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S. L. P. 10,
40479 DODOMA.

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb.Na. GA.80/145/01A/51

22 Novemba, 2023

Mwenyekiti,
TAMONGSCO,
S.L.P.63088,
DODOMA.

Katibu Mtendaji,
Christian Social Services Commission (CSSC),
S.L.P.1454,
DAR ES SALAAM

Katibu Mtendaji,
Baraza kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA),
S.L.P. 21422,
DAR ES SALAAM.

Mwenyekiti,
Tanzania Association of Private Investors in Education (TAPIE),
S.L.P.13346,
DAR ES SALAAM

Mwenyekiti,
Baraza la Sunnar Tanzania (BASUTA),
S.L.P.8581,
DAR ES SALAAM.

Mkurugenzi
Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET),
S. L. P. 13547,
DAR ES SALAAM.

Mwenyekiti,
TAWOSCO,
S. L. P. 2458,
DODOMA.

Umoja wa Wazazi Jumuiya ya CCM.

S.L.P. 3,

DODOMA.

Yah: **WARAKA WA ELIMU NA. 3 WA MWAKA 2023 KUHUSU KALENDA YA MIHULA YA MASOMO KWA SHULE ZA AWALI, MSINGI NA SEKONDARI KWA MWAKA 2024**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na idadi sahihi ya siku za masomo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeandaa **Kalenda ya Mihula ya Masomo kwa Shule za Awali, Msingi na Sekondari kwa Mwaka 2024.**
3. Ni muhimu kuzingatia utekelezaji wa Kalenda husika kwa ufanisi ili kuepuka changamoto ya kutokamilisha ufundishaji na ujifunzaji wa mada zote kwa wakati na hivyo kulazimika kuweka mipango ya ufundishaji na ujifunzaji inayowanyima watoto/wanafunzi fursa ya kupumzika na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii katika familia na jamii zao.
4. **Kalenda ya Mihula ya Masomo kwa Shule za Awali, Msingi na Sekondari kwa Mwaka 2024** ni kama ifuatavyo:

MIHULA	KUFUNGUA MUHULA	LIKIZO FUPI		KUFUNGA MUHULA	IDADI YA SIKU ZA MASOMO
		KUFUNGA	KUFUNGUA		
Muhula I	08/01/2024	28/03/2024	08/04/2024	31/05/2024	94
Muhula II	01/07/2024	30/08/2024	16/09/2024	06/12/2024	100
Jumla ya Siku za Masomo					194

Tanbihi:

- Siku za Masomo kwa mwaka ni 194.
 - Mashindano ya UMITASHUMTA yatafanyika tarehe 02/06/2024 hadi 15/06/2024, na UMISSETA yatafanyika tarehe 16/06/2024 hadi 29/06/2024.
 - Mashindano ya Michezo ya Shule za Sekondari za Afrika Mashariki (FEASSSA) yatafanyika tarehe 14/08/2024 hadi 25/08/2024 nchini Uganda.
5. Nawatakia utekelezaji mwema.



Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

KAMISHNA WA ELIMU